JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI

# SHERIA NDOGO YA (ADA NA USHURU) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI YA MWAKA 2024.

**[TANGAZO LA SERIKALI NA. 39 LA MWAKA 2024]**

TANGAZO LA SERIKALI NA. 39 la tarehe 19/1/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA (ADA NA USHURU) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI YA MWAKA 2024

Jina

1.Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"ada" maana yakeni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

chombo cha usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha abiria na mizigo kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine isipokuwa baiskeli, mkokoteni au wanyama wanaotumika kusafirisha watu au mizigo;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya

Moshi;

"hesabu" maana yake ni jumla ya mauzo ya bidhaa, kazi au huduma katika mwaka wa mapato;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"kipindi maalum cha hesabu" maana yake ni muda ambao mfanyabiashara anatakiwa kuwasilisha hesabu za biashara kwa Halmashauri;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"soko" maana yake ni ni eneo au soko liliotengwa na linalomikiwa na Halmashauri kama soko;

"hifadhi ya barabara" ina maana iliyoainishwa katika Sheria ya Barabara;

"kituo cha mabasi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo;

"ushuru" maana yake ni maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"ushuru wa huduma" maana yake ni ushuru unaotozwa au unaokusanywa na Halmashauri kutoka kwa Kampuni, tawi la Kampuni, taasisi ya biashara au mfanyabiashara kwa huduma anazopata kutokana na kutumia miundombinu ya umma inayomuwezesha kufanya biashara katika eneo la Halmashauri

"ukokotoaji" maana yake ni namna ya kuandaa kiasi cha Ushuru wa huduma kitakacholipwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

"wakala" maana yake ni kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria

Ndogo hii.

Utozaji wa ada au ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa ajili ya vibali au leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ada au ushuru

5. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Ushuru wa stendi

6. Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa ajili ya stendi na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri ndani ya stendi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Mabasi yote yatokayo na kuelekea Moshi Mjini yatalazimika kuingia katika stendi ya Njiapanda.

(3) Mabasi yote yatokayo na kuelekea Marangu, Kilema, Mamba, Mwika na Holili na yatalazimika kuingia katika stendi ya Himo.

(4) Ni marufuku kwa mabasi kupakia na kushusha abiria nje ya stendi, eneo la mizani au sehemu yeyote ambayo haijaidhinishwa na Halmashauri.

(5) Endapo dereva, utingo au mtu yeyote anayehusika na basi atagoma kilipa ushuru wa Stendi atalipa ushuru husika na faini kama ilivyo ainishwa kwenye Sheria Ndogo

hii, basi lake litakamatwa na endapo ndani ya masaa 12 hatakuwa amelipa Halmashauri itafungua kesi mahakamani na basi lake litapelekwa katika kituo cha Salama kwa uhifadhi kwa gharama za mwenye basi hadi pale basi litakapokombolewa.

Ushuru wa magulio na minada

7.-(1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa ajili ya magulio, masoko na minada na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Mtu yeyote hataruhusiwa kufanya biashara nje ya magulio, masoko na minada yaliyotengwa na Halmashauri.

Ushuru wa mazao

8.-(1) Kutakuwa na ushuru wa mazao utakaotozwa na Halmashauri kwa viwango ambavyo vimeainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii:

(a) kwa mnunuzi wa mazao pindi anunuapo mazao kutoka kwa muuzaji katika eneo la Halmashauri;
(b) kwa mnunuzi wa mazao pindi anunuapo mazao kutoka kwa muuzaji katika eneo la Halmashauri;
(c) kwa mtu yeyote atakayesafirisha mazao zaidi ya tani moja kutoka eneo lolote la Halmashauri.

(2) Halmashauri haitatoza ushuru wa mazao kwa mtu yeyote ambaye analima kwa ajili ya kujikimu na familia yake mwenye mazao yasiyozidi tani moja.

(3) Mtu yeyote atakayesafirisha mazao yasiyozidi tani moja atatakiwa kuwa na barua kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji wa sehemu aliyolima mazao yake ambayo itathibitisha kwamba mtu huyo ameyelima shamba katika Kijiji chake.

(4) Ili kuondoa mashaka, katika kupata hesabu ya tani moja yatahesabiwa magunia kumi yenye ujazo usiozidi debe nane kama ndio sawa na tani moja.

(5) Halmashauri itakuwa na Mamlaka ya kutoa mwongozo kuhusu utozaji wa ushuru wa mazao kila mwaka ambapo itaweka kiwango cha kununulia mazao kwa msimu husika ambacho kitatumika kama msingi wa utozaji wa

ushuru wa mazao kwa msimu huo.

Kibali cha kusafirisha mazao

9.-(1) Kutakuwa na kibali cha kusafirisha mazao kitakachotolewa na Halmashauri kwa mnunuzi wa mazao atakayesafirisha mazao yake nje ya eneo la Halmashauri kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

(2) Kibali hiki hakitawahusu wafanyabiashara wanaosafirisha mazao ya chakula cha mifugo kama vile pumba laini, mashudu na mazao mengine yanayoendana na hayo.

(3) Kibali chini ya kifungu hiki kitapaswa kulipiwa kiasi cha Shilingi elfu ishirini.

Ushuru wa Huduma

10.-(1) Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru wa huduma kwa kiwango cha asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya mauzo baada ya kutoa Kodi ya Ongezeko la Thamani na Ushuru wa Bidhaa kutoka kwa mtu yeyote mwenye leseni ya biashara anayewasilisha hesabu za mauzo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru wa huduma kwa kiwango kilichoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii kutoka kwa wafanyabiashara wenye leseni za biashara ambao hawawasilishi hesabu za mauzo Mamlaka ya Mapato Tanzania

(3) Itakuwa ni wajibu wa kila mfanyabiashara mwenye leseni ya biashara ambaye anawajibika kulipa ushuru wa huduma kuwasilisha kwa Mkurugenzi taarifa za hesabu za mwaka kwa ajili ya kukokotoa kiwango.

(4) Halmashauri itakokotoa ushuru wa huduma kwa walipa ushuru wa huduma wanaowasilisha taarifa za mauzo Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuzingatia taarifa zinazowasilishwa na walipa ushuru wa huduma katika kipindi maalum cha hesabu.

(5) Kila mlipa ushuru wa huduma atatakiwa kulipa

ushuru wa huduma si zaidi ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kuwasilisha taarifa za mauzo ya kila mwezi, miezi mitatu, miezi sita au miezi kumi na mbili.

Ushuru wa mazao ya misitu

11. Kutakuwa na ushuru wa mazao ya misitu utakaotozwa na Halmashauri kwa viwango ambavyo vimeainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

Ushuru wa madini ya ujenzi

12.-(1) Kila mnunuzi au msafirishaji wa madini ya ujenzi atatakiwa kulipia ushuru wa madini ya ujenzi kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii

(2) Ushuru wa madini ya ujenzi utatozwa katika eneo la machimbo, barabara zinazoelekea au kutoka maeneo ya machimbo au eneo lolote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri.

Kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi

13.-(1) Mtu yeyote anayekusudia kuanzisha machimbo ya madini ya ujenzi katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuwasilisha kwa Mkurugenzi maombi ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii.

(2) Maombi ya kibali yatatakiwa kuambatishwa na taarifa zifuatazo:

(a) leseni ya uchimbaji wa madini iliyotolewa na mamlaka husika;
(b) aina ya madini yanayokusudiwa kuchimbwa;
(c) umiliki pamoja na ukubwa wa eneo linalokusudiwa kuchimbwa madini ya ujenzi;
(d) mpango wa utunzaji wa mazingira katika eneo la machimbo; na
(e) muhtasari wa Kijiji ambacho uchimbaji wa madini ya ujenzi unafanyika ukionesha kumtambua mchimbaji.

(3) Mkurugenzi, ndani ya muda wa siku saba tangu

kupokea maombi, atatakiwa kukagua eneo ambalo uchimbaji wa madini ya ujenzi unakusudiwa kufanyika ili kujiridhisha iwapo eneo hilo linafaa kwa shughuli za uchimbaji.

(4) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Mkurugenzi baada ya kukamilika kwa ukaguzi wa eneo linaloombewa kibali atatakiwa kukubali au kukataa maombi na endapo atakataa atatoa sababu za kukataa kwa maombi hayo.

Kufutwa au kusimamishwa kwa kibali

14.-(1) Halmashauri inaweza kufuta au kusimamisha kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi endapo itajiridhisha kuwa kuna ukiukwaji wa masharti ya Sheria Ndogo hii au masharti ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri kabla ya kufuta au kusimamisha kibali itatakiwa kutoa notisi ya siku saba ya kusudio la kufuta au kusimamisha kibali kwa mtu yeyote aliyepewa kibali cha uchimbaji.

(3) Notisi itakayotolewa kwa mujibu wa Kifungu Kidogo cha (2) itaainisha sababu za kufuta au kusimamisha kibali husika.

(4) Endapo kibali kitafutwa au kusimamishwa, mtu yeyote aliyepewa kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi atasimama kuchimba madini hayo.

Ushuru wa vibali vya ujenzi

15.-(1) Mtu yeyote anayetaka kujenga, kubomoa, kuongeza au kufanya marekebisho makubwa yanayoweza kuathiri uimara wa jengo atatakiwa kupata kibali cha ujenzi.

(2) Ada na ushuru wa vibali vya ujenzi itatozwa kama ilivyo ainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(3) Kila mtu anayeomba kibali cha ujenzi atajaza fomu ya maombi ya kibali cha ujenzi na kuambatanisha nyaraka zote zinazotakiwa kuwasilishwa.

(4) Muda wa kibali cha ujenzi ni miezi sita kuazia tarehe ya kutolewa kwa kibali cha ujenzi.

Timu ya kuidhinisha vibali vya ujenzi

16.-(1) Kutakuwa na timu ya wataalamu ya kuidhinisha vibali vya ujenzi itakayoundwa na Mkurugenzi Mtendaji. ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mkurugenzi Mtendaji;
(b) Afisa Ardhi;
(c) Mpima Ardhi;
(d) Afisa Mipango Miji;
(e) Msanifu au Mbunifu Majengo;
(f) Mhandisi wa Ujenzi;
(g) Afisa Mazingira;
(h) Afisa anyesimamia Anuani za Makazi; na
(i) Mthamini Ardhi.

(2) Mwenyekiti wa Timu ya Wataalamu atakua Mkurugenzi Mtendaji na katibu wa Timu ya Wataalamu atakua Mhandisi wa Ujenzi.

Ushuru wa utalii

17. Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru katika lango kuingia kwenye eneo la utalii kwa mtu yeyote au chombo cha usafiri kwa viwango vilivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

Ushuru wa nyumba za kulala wageni

18.-(1) Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru wa nyumba za kulala wageni kwa kiwango cha asilimia kumi ya bei ya chumba kwa siku kwa nyumba za kulala wageni ambayo haijasajiliwa kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani.

(2) Kila mlipa ushuru wa nyumba ya kulala wageni anatakiwa kuwa na daftari maalum kwa ajili ya kuorodhesha wageni wanaoingia kupata huduma ya malazi.

(3) Kila mlipa ushuru atatakiwa kuwasilisha Halmashauri taarifa sahihi ya idadi ya wageni kwa kila chumba kilichopangishwa pamoja na ushuru wa nyumba ya kulala wageni kwa kila mwisho wa mwezi.

(4) Endapo itabainika kuwa kuna mgeni au wageni ambao hawajaorodheshwa katika daftari maalum la wageni, Halmashauri itakuwa na mamlaka kisheria ya kumtoza

mmiliki huyo ushuru kwa kiwango cha idadi ya vyumba vyote vya hoteli hiyo.

Ushuru wa mabango ya biashara

19. Halmashauri itatoza ada au ushuru wa mabango ya biashara utakaotozwa kutoka kwa wafanyabiashara kwa viwango ambavyo vimeainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

Muda wa kukusanya ada au ushuru

20.-(1) Muda wa kukusanya ada au ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda uliotajwa katika kifungu kidogo cha (1).

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ada au ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Ukusanyaji wa madeni

21.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya Mahakama endapo mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni itakuwa imeshindwa kulipa ada au ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika Kifungu kidogo cha (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya kipindi cha siku thelathini kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata

idhini ya Mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(5) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika Kifungu Kidogo cha (3) na (4), Halmashauri kabla ya kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote ile itakayotokea ama wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri au wakala.

Uteuzi wa Wakala

22.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii;

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

23. Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Kamati ya kufuatilia mapato

24.-(1) Kutakuwa na Kamati yakufatilia mapato ya Halmashauri itakayoundwa na Mkurugenzi ambayo itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kuratibu utendaji kazi wa kikosi kazi cha kukusanya mapato;
(b) kuishauri Halmashauri kuhusu namna ya kuongeza mapato na kubuni vyanzo vipya vya mapato;
(c) kufanya tathmini ya makusanyo katika kila chanzo kwa mwaka ili kuweka maoteo ya mwaka unaofuata.

(2) Kamati ya mapato itawajibika kutoa taarifa ya utendaji kazi kwa Menejimenti kila mwezi kuonyesha namna ilivyofanya kazi katika kipindi husika.

Kikosi kazi cha kudhibiti mapato

25.-(1) Kutakuwa na kikosi kazi cha kufuatilia na kudhibiti utoroshaji wa mapato ambacho kitaundwa na Mkurugenzi kikihusisha wataalamu kutoka sekta mbalimbali za Halmashauri.

(2) Kikosi kazi kitakachoundwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kitawajibika kwa Kamati ya Mapato.

Makosa

26. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo;

(a) atashindwa au atadharau au atakwepa au atakataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii
(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;
(c) atamzuia Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(d) atatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri;

(e) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ushuru na zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri;

(f) atatumia chombo chochote kile kusafirishia bidhaa ambayo haijalipiwa ushuru au ada;

(g) atashindwa kuwasilisha hesabu sahihi za biashara yake;

(h) atashindwa kuwasilisha nyaraka, maelezo au taarifa inayotakiwa kuwasilishwa kwa Mkurugenzi au Afisa mwidhiniwa katika muda uliowekwa;

(i) atashindwa kutunza kumbukumbu yoyote au nyaraka kwa ajili ya ukokotoaji wa mahesabu ya ushuru wa huduma;

(j) ataandaa au kutengeneza au kusababisha kuandaliwa au kutengenezwa kwa vitabu vya uongo vya hesabu au kumbukumbu

Adhabu

27. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote kwa Pamoja.

Kufililisha kosa

28. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Nne la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa TS Na. 160 la mwaka

Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Mwaka 2014 na Sheria Ndogo ya (Kodi ya Huduma) ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Mwaka 2008

2014
236 la
mwaka
2008

zinafutwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 4(1))*

SEHEMU YA KWANZA

ADA YA VIBALI VYA SHEREHE, MATANGAZO, BURUDANI NA SHUGHULI ZA UTAMADUNI

1. Ada ya Sherehe

| Namba | Aina ya huduma | Kiwango cha malipo (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Sherehe za Vijijini | 30,000/= kwa siku |
| 2. | Sherehe za Mjini (Maeneo ya Mipangomiji) | 50,000/= kwa siku |

2. Ada za Matangazo

| Namba | Aina ya huduma | Kiwango cha malipo (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Promotion | 50,000/= kwa siku |
| 2. | Mnada wa bidhaa | 50,000/= kwa siku |

3. Burudani

| Namba | Aina ya huduma | Kiwango cha malipo (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Mshereheshaji (MC) | 10,000/= kwa siku |
| 2. | Mchezesha Muziki (DJ) | 10,000/= kwa siku |
| 3. | Mapambo | 10,000/= kwa siku |
| 4. | Mzabuni wa Chakula | 10,000/= kwa siku |
| 5 | Mzabuni wa Vinywaji | 10,000/= kwa siku |
| 7 | Night Club | 200,000/= kwa mwaka |
| 8. | Vibanda vya burudani (vibanda umiza) | 10,000/= kwa mwezi |
| 9. | Muziki wa bendi | 30,000/= kwa siku |
| 10. | Burudani ya kandanda | 1,000/= kwa mtu mzima, na 500/= kwa mtoto. |
| 11. | Burudani ya ngumi (mwandaaji) | 50,000/= kwa siku |

| | | |
|---|---|---|
| 12. | Ada ya usajili na vibali wa kumbi za burudani | 25% ya usajili ya Gharama ya Usajili BASATA |
| 13. | Usajili na vibali wa vikundi vya sanaa | 20% ya usajili ya Gharama ya Usajiri |
| 14. | Usajili na vibali wa vyama au vilabu vya michezo | 20% ya usajili ya Gharama ya Usajili |
| 15. | Kibali cha kuchezesha disco au Maonyesho ya bendi au Sanaa za maonyesho (Sinema au picha mjongeo au maigizo au sarakasi au ada nyingine | 50,000/= kwa tukio |
| 16. | Kibali cha mchezo wa pool table | 50,000/=kwa mwaka. |
| 17. | Kibali cha tamasha au kongamano na mikutano ya kidini nje ya sehemu za kuabudia. | 20,000/= kwa siku |
| 18. | Bahati nasibu ndogo ndogo (fete) | 10,000/= kwa kwa mwezi |
| 19. | Kibali cha matangazo | 50,000/= kwa tangazo ya biashara. |
| 20. | Kibali cha Mazishi | Bure |

## SEHEMU YA PILI

### ADA YA KUKODI MALI ZA HALMASHAURI

| Namba. | Aina | Kiwango cha Ada |
|---|---|---|
| 1. | Ukumbi wa Halmashauri | Kodi ya pango itatajwa kwenye mkataba |
| 2 | Nyumba za Halmashauri | Kodi ya pango itatajwa kwenye mkataba. |
| 3. | Vibanda vya biashara vya Halmashauri | Kodi ya pango itatajwa kwenye mkataba. |
| 4. | Meza za Sokoni | Kodi ya pango itatajwa kwenye mkataba. |
| 5. | Magari na Mitambo | Kodi ya pango itatajwa kwenye mkataba. |
| 6. | Kukodi vitalu vya kufugia mifugo | Kodi ya pango itatajwa kwenye mkataba. |
| 7. | Mali nyingine ya Halmashauri | Kodi ya pango itatajwa kwenye |

| | | |
|---|---|---|
| | | mkataba. |

SEHEMU YA TATU

ADA YA HUDUMA YA MAGHALA YA HALMASHAURI

| Namba | Aina ya huduma | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kutunza dagaa kwenye ghala | 500/= kwa kila gunia kwa siku |
| 2. | Kutunza samaki wakavu | 15/= kwa kilo |
| 3. | Kutunza bidhaa nyinginezo | 500/= kwa kila gunia kwa siku |

SEHEMU YA NNE

ADA AU USHURU WA UKAGUZI WA AFYA

| Namba | Aina ukaguzi | Kiwango cha malipo (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba za starehe (baa,vilabu vya pombe za kienyeji na nyumba ya kulala wageni | 3,000/= kila baada ya miezi mitatu |
| 2. | Nyumba ya kutengeneza na kuuzia vyakula au nyama choma. | 3,000/= kila baada ya miezi mitatu |
| 4. | Maombi ya kufungua Biashara baada ya ukaguzi ili kufunguliwa upya | 15,000/= mara moja. |
| 5. | Ukaguzi wa viwanda vikubwa | 150,000/= kwa mwaka |
| 6. | Ukaguzi wa viwanda vya kati | 100,000/= kwa mwaka |
| 7 | Ukaguzi wa viwanda vidogo | 50,000/= kwa mwaka |

| | | |
|---|---|---|
| 8. | Upimaji afya wahudumu | 5,000/= kila baada ya miezi mitatu |

SEHEMU YA TANO

ADA YA USAJILI WA TEKSI, MAGARI YA MIZIGO, PIKIPIKI NA PIKIPIKI ZA MAGURUDUMU MATATU

| Namba. | Aina ya Gari | Ukubwa | Kiasi cha ushuru kwa mwaka (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Teksi | - | 60, 000/= |
| 2. | Magari ya mizigo | chini ya tani moja na nusu | 30,000/= |
| 3. | Magari ya mizigo | zaidi ya tani moja na nusu | 40,000/= |
| 4 | Pikipiki | - | 17,000/= |
| 5 | Pikipiki ya Magurudumu Matatu (Bajaji) | - | 22,000/= |

SEHEMU YA SITA

USHURU WA KUINGIA NA MAEGESHO NA NDANI YA KITUO CHA MABASI

| Namba | Aina ya chombo cha usafiri | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Gari au basi kubwa | 2,000/= kwa siku |
| 2. | Magari madogo (Hiace) | 1,000/= kwa siku |
| 3. | Teksi | 1,000/= kwa siku |

| | | |
|---|---|---|
| 4. | Bajaji au Guta au mkokoteni | 500/= kwa siku |
| 5. | Magari binafsi yasiyo ya biashara | 500/= kila linapotoka stendi |
| 6. | Gari dogo la mizigo (Lori au Pick – up) chini ya Tani 7 | 2,000/= kila linapotoka stendi |
| 7. | Gari kubwa la mizigo zaidi ya Tani 7 | 3,000/= kila linapotoka stendi |
| 8. | Kuingia ndani ya Standi au kituo cha mabasi kwa mtu asiye na tiketi | 200/= kila anapoingia. |

SEHEMU YA SABA

USHURU WA KULAZA VYOMBO VYA USAFIRI KATIKA MAENEO YALIYOTENGWA NA HALMASHAURI

| Namba | Aina ya chombo cha usafiri | Kiwango cha ushuru(Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Gari (Lori)kubwa la mizigo | 5,000/= kwa siku |
| 2. | Fuso au kenta au magari mengine ya mizigo | 3,000/= kwa siku |
| 3. | Basi kubwa | 3,000/= kwa siku |
| 4 | Mabasi ya kati | 2,000/= kwa siku |
| 5. | Teksi | 1,000/= kwa siku |
| 6 | Magari binafsi yasiyo ya biashara | 1,000/= kwa siku |
| 7. | Aina nyingine ya chombo cha usafiri | 1,000/= kwa siku. |

SEHEMU YA NANE

USHURU WA MAGULIO, MASOKO NA MINADA

| Namba | Aina ya biashara | Kiwango cha ushuru(Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Biashara ya nguo za mitumba | 1,000/= kwa siku |
| 2. | Biashara ya nguo za madukani | 1,000/= kwa siku |
| 3. | Biashara ya viatu vya mitumba | 1,000/= kwa siku |
| 4. | Biashara ya vileo | 2, 000/= kwa siku |
| 5. | Biashara ya kuuza nyama choma | 2,000/= kwa siku |
| 6. | Michezo mbalimbali katika soko | 2,000/= kwa siku |
| 7. | Biashara za bidhaa za urembo | 1,000/= kwa siku |
| 8. | Biashara ya vyombo vya ndani | 1,000/= kwa siku |
| 9. | Biashara ya samani mbalimbali | 1,000/= kwa siku |
| 10. | Biashara nyingine | 1,000/= kwa siku |
| 11. | Meza za nafaka na samaki wabichi | 1,000/= kwa siku |
| 12. | Wauza kuku vibandani | 500/= kwa siku |

SEHEMU YA TISA

USHURU WA MAEGESHO KATIKA MASOKO, NA MAENEO MENGINE YA HALMASHAURI

| Namba | Aina ya chombo cha usafiri | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Gari lenye ndizi,Viazi na mazao ya nafaka tani 1 hadi 4 | 10,000/= kwa tripu |
| 2. | Gari lenye bidhaa za viwandani tani 1 hadi 4 | 15,000/= kwa tripu |
| 3 | Gari lenye ndizi,Viazi na mazao ya nafaka tani 5 na kuendelea | 15,000/= kwa tripu |
| 4 | Gari lenye bidhaa za viwandani tani 5 na kuendelea | 20,000/= kwa tripu |
| 5. | Gari la mafuta ya taa, dizeli au petrol zaidi ya tani 10 | 25,000/= kwa tripu |
| 6. | Gari la mafuta ya taa, dizeli au petroli chini ya tani 10 | 20,000/= kwa tripu |
| 7. | Gari la gesi na bidhaa nyingine zenye mlipuko | 30,000/= kwa tripu |
| 8. | Gari la bidhaa nyinginezo | 1,000/= kwa tripu |

SEHEMU YA KUMI

ADA YA HUDUMA YA VYOO VYA HALMASHAURI

| Namba | Aina ya Jengo | Kiasi (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Choo cha Stendi | 300/= kwa kila mtu |
| 2. | Choo cha Soko kuu | 300/= kwa kila mtu |
| 3 | Choo cha Soko, Gulio na Mnada | 200/= kwa kila mtu |

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA

### USHURU WA MAZAO.

| Namba | Aina ya mazao | Kiwango cha ushuru(Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Mazao ya Chakula | 3% ya bei ya kununulia (mauzo) |
| 2. | Mazao ya Biashara | 3% ya bei ya kununulia (mauzo) |

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI

### ADA/USHURU WA MAGANDA YA KAHAWA KWENDA NJE YA HALMASHAURI

| Namba | Aina ya chombo cha usafiri | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Gari tani 1-10 | 10,000/= kwa safari(tripu) |
| 2. | Gari tani 11-30 | 20,000/= kwa safari(tripu) |

## SEHEMU YA KUMI NA TATU

### USHURU WA HUDUMA KWA WAFANYA BIASHARA WENYE LESENI ZA BIASHARA AMBAO HAWAWASILISHI HESABU ZA MAUZO MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA)

| Namba. | Aina ya Bishara | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Bahati Nasibu (Mashine) | 50,000/= |
| 2. | Duka la kuoka mikate | 100,000/= |
| 3. | Biashara ya Kuuza mifugo | 150,000/= |
| 4. | Duka la nyama | 80,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 5. | Cable TV Networks | 200,000/= |
| 6. | Sehemu ya kuoshea magari/pikipiki | 100,000/= |
| 7. | Day Care & Nursery School | 200,000/= |
| 8. | Driving School | 300,000/= |
| 9. | Duka la vifaa vya ofisini/Kupiga chapa. | 80,000/= |
| 10. | Duka la Bia za Jumla | 300,000/= |
| 11. | Duka la dawa baridi | 50,000/= |
| 12. | Duka la ku burn na kuuza CD/Flash | 30,000/= |
| 13. | Duka la kushona nguo | 30,000/= |
| 14. | Duka la kuuza computer/Radio | 100,000/= |
| 15. | Duka la kuuza magodoro | 50,000/= |
| 16. | Duka la kuuza Maua | 30,000/= |
| 17. | Duka la kuuza mitungi ya gesi na majiko | 100,000/= |
| 18. | Duka la kuuza nguo | 50,000/= |
| 19. | Duka la kuuza vilainishi vya vyombo vya usafiri. | 50,000/= |
| 20. | Duka la kuuza pembejeo za kilimo | 60,000/= |
| 21. | Duka la kuuza viatu | 50,000/= |
| 22. | Duka la kuuza vifaa vya Maabara | 100,000/= |
| 23. | Duka la kuuza vifaa vya simu | 60,000/= |
| 24. | Duka la kuuza Vifaa vya Umeme | 150,000/= |
| 25. | Duka la vifaa vya maji | 100,000/= |
| 26. | Duka la vipuri vya magari | 150,000/= |
| 27. | Duka la vipuri vya pikipiki/baiskeli | 60,000/= |
| 28. | Duka la vinyago | 100,000/= |
| 29. | Duka la vipodozi | 50,000/= |
| 30. | Duka la vyakula vya mifugo | 60,000/= |
| 31. | Duka la vyombo | 50,000/= |
| 32. | Fundi wa kuranda | 70,000/= |
| 33. | Fundi wa vifaa vya umeme na kieletroniki | 70,000/= |
| 34. | Karakana ya magari. | 80,000/= |
| 35. | Bustani | 300,000/= |
| 36. | Ghala la kuhifadhia mazao | 150,000/= |
| 37. | Duka la vifaa vya Ujenzi | 300,000/= |
| 38. | Kituo cha Kulea na Kutunza watoto | 150,000/= |
| 39. | Kioski | 40,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 40. | Karakana | 70,000/= |
| 41. | Kufyatua matofali | 100,000/= |
| 42. | Kukamua mafuta ya alizeti | 40,000/= |
| 43. | Kuloweka mbege | 50,000/= |
| 44. | Kupiga picha | 30,000/= |
| 45. | Kushona nguo(Mashine moja) | 30,000/= |
| 46. | Kuuza Samaki | 80,000/= |
| 47. | Maabara | 100,000/= |
| 48. | Machinjio | 150,000/= |
| 49. | Maduka ya RejaReja | 50,000/= |
| 50. | Mafundi wa Kutengeneza mizani | 200,000/= |
| 51. | Mashine ya kukoboa Mpunga | 150,000/= |
| 52. | Mgahawa | 30,000/= |
| 53. | Migodi ya Madini ya Ujenzi | 300,000/= |
| 54. | Milling machine/Mashine ya kukoboa na Kusaga nafaka | 30,000/= |
| 55. | Mwika SIDO- (KIWANDA) | 500,000/= |
| 56. | Private Students Hostel | 150,000/= |
| 57. | Saloni | 30,000/= |
| 58. | Social Hall Ukumbi | 300,000/= |
| 59. | Sonara | 150,000/= |
| 60. | Studio | 80,000/= |
| 61. | Super Market | 150,000/= |
| 62. | Timber Yard | 150,000/= |
| 63. | Wakala wa Fedha(Mpesa,Tigo Pesa) | 50,000/= |
| 64. | Welding | 70,000/= |
| 65. | Whole sale | 300,000/= |
| 66. | Workshop ya kuranda mbao | 70,000/= |

______________

SEHEMU YA KUMI NA NNE

______________

ADA/USHURU WA MAZAO YA MISTU

| Namba | Aina ya zao | Kiasi cha malipo(Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Mbao za asili | 3% ya thamani ya ubao |

| | | |
|---|---|---|
| 2 | Mbao za kupandwa | 300/= kwa kila ubao |
| 3 | Mkaa | 1,000/= kwa kila gunia |
| 5 | Asali | 300/= kwa kila kilo |
| 6 | Slipa | 100/= kwa kila slipa |
| 7 | Kitanda kipya | 1,000/= kwa kila kitanda |
| 8 | Kiti | 500/=kwa kiti kimoja |
| 9 | Kochi dogo | 500/= kwa kochi |
| 10 | Kochi kubwa | 1,000/= kwa kochi |
| 11 | Kuni | 20,000/= Chini y a Tani 7, |
| 12 | Kuni | 25,000/= zaidi ya Tani 7, |
| 13 | Meza | 1,000/= kwa kila meza |
| 14 | Frame ya mlango | 2,000/= kwa kila fremu ya mlango |
| 15 | Shutter(Top) | 2,000/= kwa kila shutter ya mlango |
| 17 | Mbao (scant) | 1,000/= kwa kila scant |
| 18 | Magogo | 1,500 kwa kila gogo. |
| 19 | Mirunda | 1,000/= kwa mrunda mmoja |
| 20 | Nguzo | 1,000 kwa kila nguzo |
| 21 | Bidhaa nyingine za ti-mbao( non wood) | 500 kwa kila bidhaa |

## SEHEMU YA KUMI NA TANO

### A. USHURU WA MAWE, MORAMU, MCHANGA NA KIFUSI

| Namba. | Uzito | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Chini ya Tani 1 kwa Tripu moja | 1,000/= |
| 2 | Zaidi yaTani 1 hadi Tani 4 kwa Tripu moja | 5,000/= |
| 3 | Zaidi ya Tani 4 hadi Tani 8 kwa Tripu moja | 10,000/= |
| 4 | Zaidi ya Tani 8 hadi Tani 15 kwa Tripu moja | 15,000/= |
| 5 | Zaidi ya Tani 16 Kuendelea kwa Tripu moja | 20,000/= |

B. USHURU WA KOKOTO, TOFALI ZA KUCHOMA, TOFALI ZA MWAMBA NA TOFALI ZA MORAMU NA MADINI MENGINE.

| Namba | Uzito | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Chini ya Tani 1 kwa Trip moja | 2,000/= |
| 2 | Zaidi ya Tani 1 hadi Tani 4 kwa Trip moja | 10,000/= |
| 3 | Zaidi ya Tani 4 hadi Tani 8 kwa Trip moja | 15,000/= |
| 4 | Zaidi ya Tani 8 hadi Tani 15 kwa Trip moja | 20,000/= |
| 5 | Zaidi ya Tani 15 na Kuendelea kwa Trip moja | 25,000/= |

C. KIBALI CHA KUMILIKI ENEO LA KUCHIMBA MADINI YA UJENZI

| Namba | Ukubwa wa Eneo | Kiwango cha Malipo (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Eneo lenye ukubwa chini ya mita za mraba 40,000 | 50,000/= kwa mwaka |
| 2. | Eneo lenye ukubwa zaidi ya mita za mraba 40,000 | 100,000/= kwa mwaka |

---

SEHEMU YA KUMI NA SITA

---

A. GHARAMA ZA VIBALI VYA UJENZI – MAENEO YALIOPIMWA

| Namba | Aina ya Ada | AINA YA JENGO | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Jengo la makazi lisilo la ghorofa | Jengo la makazi la ghorofa | Jengo la biashara lisilo la ghorofa | Jengo la biasharala ghorofa | Majengo ya shule | Majengo ya nyumba za ibada |
| 1. | Ada ya Ukaguzi | Shilingi 2,500/= | Shilingi 2,500/= | Shilingi 2,500/= | Shilingi 2,500/= | Shilingi 2,500/= | Shilingi 2,500/= |
| 2. | Ada ya | Shilingi | Shilingi | Shilingi | Shilingi | Shilingi | Shilingi |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kibali cha Ujenzi | 300/= kwa mita moja ya mraba | 300/= kwa mita moja ya mraba | 300/= kwa mita moja ya mraba | 300/= kwa mita moja ya mraba ya sakafu | 100/= kwa mita moja ya mraba | 100/= kwa mita moja ya mraba |

B. GHARAMA ZA VIBALI VYA UJENZI – MAENEO YA VIJIJINI

| Namba | Aina ya ada | AINA YA JENGO | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Jengo la makazi lisilo la ghorofa | Jengo la makazi la ghorofa | Jengo la biashara lisilo la ghorofa | Jengo la biasharala ghorofa | Majengo ya shule | Majengo ya nyumba za ibada |
| 1. | Ada ya Ukaguzi | Shilingi 2,000/= | Shilingi 2,000/= | Shilingi 2,000/= | Shilingi 2,000/= | Shilingi 2,000/= | Shilingi 2,000/= |
| 2. | Ada ya Kibali cha Ujenzi | Shilingi 200/= kwa mita moja ya mraba | Shilingi 200/= kwa mita moja ya mraba | Shilingi 200/= kwa mita moja ya mraba | Shilingi 200/= kwa mita moja ya mraba ya sakafu | Shilingi 50/= kwa mita moja ya mraba | Shilingi 50/= kwa mita moja ya mraba |

B. UJENZI MAALUM

| Namba | Aina ya Ujenzi | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Kituo cha Mafuta | 500,000/= |
| 2 | Minara ya Mawasiliano (Simu, Radio na Tv) | 1,500,000/= |
| 3 | Kuhuisha Kibali cha Ujenzi | 50,000/= |

C. ADA YA MABADILIKO YA NYUMBA AU JENGO LILILOPO

| Namba. | Aina | Kiwango cha Ada(Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba ya makazi | 10,000/= |
| 2. | Nyumba ya biashara | 15,000/= |
| 3 | Ghorofa | 100,000/= |
| 4. | Kiwanda, bohari ghala | 100,000/= |
| 5. | Kituo cha mafuta | 100,000/= |
| 6. | Maombi ya kugawanya ardhi | 100,000/= |
| 7. | Majengo mengine | 10,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA SABA

A. VIVUTIO VYA ASILI

| Namba. | Aina ya Utalii | Mwanafunzi Shule ya Msingi (Shilingi) | Mwanafunzi Shule ya Sekondari (Shilingi) | Mwanafuzi wa Chuo (Shilingi) | Mtu Mzima Mtanzania (Shilingi) | Mwanafunzi Nje ya Nchi (Shilingi) | Mtu Mzima Nje ya Nchi. (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Hifadhi ya wanyama pori | 500/= | 1,000/= | 2,000/= | 5,000/= | 5,000/= | 10,000/= |
| 2 | Fukwe | 500/= | 1,000/= | 2,000/= | 5,000/= | 5,000/= | 10,000/= |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 3 | Mahandaki | 500/= | 1,000/= | 2,000/= | 5,000/= | 5,000/= | 10,000/= |
| 4 | Maanguko ya Maji | 500/= | 1,000/= | 2,000/= | 5,000/= | 5,000/= | 10,000/= |
| 5 | Milima | 500/= | 1,000/= | 2,000/= | 5,000/= | 5,000/= | 10,000/= |
| 6 | Misitu | 500/= | 1,000/= | 2,000/= | 5,000/= | 5,000/= | 10,000/= |
| 7 | Maeneo Tengefu | 500/= | 1,000/= | 2,000/= | 5,000/= | 5,000/= | 10,000/= |

B. VIVUTIO VYA KUTENGENEZA

| Namba. | Aina ya Utalii | Mwanafunzi Shule ya Msingi (Shilingi) | Mwanafunzi Shule ya Sekondari (Shilingi) | Mwanafuzi wa Chuo (Shilingi) | Mtu Mzima Mtanzania (Shilingi) | Mwanafunzi Nje ya Nchi (Shilingi) | Mtu Mzima Nje ya Nchi. (Shiling) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Sehemu ya Burudani | 500/= | 1,000/= | 2,000/= | 5,000/= | 5,000/= | 10,000/= |
| 2 | Banda la wanyamapori (Zoo) | 500/= | 1,000/= | 2,000/= | 5,000/= | 5,000/= | 10,000/= |
| 3 | Makumbusho na makusanyo ya Picha | 500/= | 1,000/= | 2,000/= | 5,000/= | 5,000/= | 10,000/= |
| 4 | Maeneo ya Kipekee | 500/= | 1,000/= | 2,000/= | 5,000/= | 5,000/= | 10,000/= |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 5 | Maeneo ya Kihistoria | 500/= | 1,000/= | 2,000/= | 5,000/= | 5,000/= | 10,000/= |

C. MICHEZO

| Namba | Aina ya Utalii | Mwanafunzi Shule ya Msingi (Shilingi) | Mwanafunzi Shule ya Sekondari (Shilingi) | Mwanafuzi wa Chuo (Shilingi) | Mtu Mzima Mtanzania (Shilingi) | Mwanafunzi Nje ya Nchi (Shilingi) | Mtu Mzima Nje ya Nchi. (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mshabiki | 500/= | 1,000/= | 2,000/= | 5,000/= | 5,000/= | 10,000/= |
| 2 | Mshiriki wa Michezo | 500/= | 1,000/= | 2,000/= | 5,000/= | 5,000/= | 10,000/= |
| 3 | Utembeleaji wa Viwanja vya Michezo | 500/= | 1,000/= | 2,000/= | 5,000/= | 5,000/= | 10,000/= |

D. MATUKIO MAALUM

| Namba. | Aina ya Utalii | Mwanafunzi Shule ya Msingi (Shilingi) | Mwanafunzi Shule ya Sekondari (Shilingi) | Mwanafuzi wa Chuo (Shilingi) | Mtu Mzima Mtanzania(Shilingi) | Mwanafunzi Nje ya Nchi (Shilingi) | Mtu Mzima Nje ya Nchi. (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Masoko | 500/= | 1,000/= | 2,000/= | 5,000/= | 5,000/= | 10,000/= |
| 2 | Tamasha la Halaiki | 500/= | 1,000/= | 2,000/= | 5,000/= | 5,000/= | 10,000/= |
| 3 | Uzindu | 500/= | 1,000/= | 2,000/= | 5,000/= | 5,000/= | 10,000/ |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | zi | | | | | | = |
| 4 | Mbio za Magari kila Mshiriki | Haruhusiwi Kushiriki | Haruhusiwi Kushiriki | 15,000/= | 20,000/= | 25,000/= | 30,000/= |
| 5 | Mbio za pikipiki kila Mshiriki | Haruhusiwi Kushiriki | Haruhusiwi Kushiriki | 10,000/= | 15,000/= | 20,000/= | 25,000/= |
| 6 | Mbio za Baisikeli kila Mshiriki | 5,00/= | 1,000/= | 2,000/= | 5,000/= | 8,000/= | 10,000/= |

E. SHUGHULI YEYOTE YA UTALII AMBAYO HAIJATAJWA KWENYE SHERIA NDOGO HII

| Mwanafunzi Shule ya Msingi (Shilingi) | Mwanafunzi Shule ya Sekondari (Shilingi) | Mwanafuzini wa Chuo (Shilingi) | Mtu Mzima Mtanzania (Shilingi) | Mwanafunzi Nje ya Nchi (Shilingi) | Mtu Mzima Nje ya Nchi. (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|---|
| 500/= | 1,000/= | 2,000/= | 5,000/= | 5,000/= | 10,000/= |

---

SEHEMU YA KUMI NA NANE

---

A. . UTUAJI WA HELIKOPTA KWENYE VIWANJA NA MAENEO YA WAZI YA HALMASHAURI

| Namba | Huduma | Muda | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Utuaji wa | Dakika 1 hadi saa | 100,000/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Helikopta | moja | |
| | | | |

B. MIKUSANYIKO KWENYE VIWANJA NA MAENEO YA WAZI YA HALMASHAURI

| Namba | Huduma | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mikusanyiko kwenye viwanja na maeneo ya wazi ya Halmashauri | 50,000/= Kwa siku |
| Zingatia: Ada hii haijumuishi ada ya kibali cha kusanyiko ambayo hutolewa na Halmashauri. | | |

SEHEMU YA KUMI NA TISA

ADA NA USHURU WA MABANGO YA BIASHARA

| Namba | Aina ya Bango | Kiwango (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Bango lisilo la Mng'ao (Non-Illuminated Sign) | 7,000/= Kwa Kila Futi Moja ya Mraba |
| 2 | Bango Mng'ao (Illuminated Sign) | 10,000/= Kwa Kila Futi Moja ya Mraba |
| 3 | Mabango ya Biashara yaliandikwa na kuchora kwenye kuta za Majengo (Wall Sign) | 10,000/= Kwa Kila Futi Moja ya Mraba. |
| 4 | Mabango ya Kietroniki (Electronic Sign) | 10,000/= Kwa Kila Futi Moja ya Mraba. |
| 5 | Bango kwenye Gari (Vehicular advertisement) | 10,000/= Kwa Kila Futi Moja ya Mraba. |
| 6 | Bango kwenye gari kwa mmiliki wa gari anayetangaza biashara yake mwenyewe (Vehicular Advertisement branding own products) | 4,000/= Kwa Kila Futi Moja ya Mraba. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7 | Bango kwenye eneo la Biashara (Point of sale display): | | |
| | (a) | Bango lisilo la Mng'ao (Non illuminated) | 7,000/= Kwa Kila Futi Moja ya Mraba. |
| | (b) | Bango Mng'ao (Illuminated) | 10,000/= Kwa Kila Futi Moja ya Mraba. |
| 8 | (i) | Mabango ya kukuza Biashara kwa mabango 100 ya awali kwa kila bango (Every poster promotion for first 100 posters). | 50,000/= |
| | (ii) | Mabango ya kukuza Biashara kwa mabango 100 ya kundi lingine kwa kila bango (For every other bunch of 100 posters or part thereof). | 50,000/= |
| 9 | (Matangazo ya muda mfupi kwa siku (Short term advertisement or promotion per day). | | 50,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA SHIRINI

ADA AU USHURU MWINGINE

| Namba | Aina ya Biashara | Kiasi (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Karakana ya uvunaji mkaa, mbao na kuni | 20% ya tozo ya Serikali Kuu Usajili kwa mwaka |
| 2 | Biashara ya bucha ya wanyamapori | 20% ya tozo ya Serikali Kuu Usajili kwa mwaka |
| 3 | Tathimini ya athari ya mazingira | 20,000/= kwa kila kazi kwa kibali |
| 4 | Shughuli za uwindaji | 20% ya tozo ya Serikali Kuu kwa mwaka |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 9(1))*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI

<u>KIBALI CHA KUSAFIRISHA MAZAO NJE YA WILAYA</u>
(Transportation Permit for Crop Produce Outside the District)

Namba ya Kibali (Permit No.) …………………………………….
Tarehe ya Kutolewa (Date of Issue) ……………………………….
Jina la Msafirishaji (Transporter's Name) …………………………
Aina ya Gari (Vehicle Type) ……………………………………….
Namba ya Gari (Vehicle Registration No.) …………………………

1. Kibali kimetolewa kwa (Permit is hereby granted to) ………………………………….. kusafirisha(To transport)………………………Tani(Tones)…………………….kutoka(From)……………..kwenda (To)……………………………..
2. Kibali hiki ni cha siku (This Permit is valid for number of days)..................kuanzia tarehe ( starting from)………………..mpaka (To)……………………..
3. Kibali hiki hakihamishiki (Not transferable)

KWA MATUMIZI YA OFISI TU (For office use only)
Namba ya kibali (Permit No.) ……………. Tarehe (Date).......................Mahali (Place)…………….
Stakabadhi Na. (Receipt No.) ………………………ya Tarehe (Date)………………………….

Jina la Afisa Muidhinishaji (Name of Authorizing Officer) ………………………………….

Saini (Signature)……………………cheo (Designation)………………………….
Muhuri (official stamp)

---

JEDWALI LA TATU

---

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 13(1))*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI

KIBALI CHA UCHIMBAJI WA MADINI YA UJENZI

Kibali hiki kimetolewa kwa Bw/Bi: ................................................................................ wa S.L.P…................. , Mlimba. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ameridhia Ndugu mtajwa hapo juu, aendeshe shughuli za kuchimba madini ya ujenzi katika eneo la …………………………Kijiji cha………………………. kata ya …………………………… baada ya kufanya ukaguzi katika eneo husika ili kutathimini athari za Mazingira.

Kutokana na uzingatiaji wa athari za mazingira mchimbaji anaruhusiwa kuchimba madini ya ujenzi katika eneo hilo kwa muda wa miezi kumi na mbili tu. mwombaji analazimika kuomba tena kibali baada ya muda huo kuisha na ukaguzi utafanyika tena.

TAMKO LA MWOMBAJI;

MIMI………………………………………………………nipo tayari kufuata masharti ya kibali hiki cha uchimbaji wa madini ya ujenzi ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kwa lengo la kutunza na kuhifadhi mazingira. Nathibitisha kwa hiari yangu nimeelewa vema masharti ya kibali hiki.

Jina: ……………………………………… Saini …………………..T arehe …………………

*KWA MATUMIZI YA OFISI;*

Mwombaji amelipia Shilingi ……………. tarehe……….mwezi………….Mwaka…………..
(Ambatanisha stakabadhi ya malipo na fomu hii)

Jina la Afisa aliyetoa kibali……………………… Saini …………… Tarehe ……………….
Muhuri:…………………………………………….

---

JEDWALI LA NNE

---

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 28)*

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi …………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Moshi, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kifungu cha …… cha Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ya mwaka, 2023.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, niko tayari kulipa kiasi cha Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….
Jina……………………………….. Saini………………………

MBELE YANGU :
Jina:…………………………………..……………………
Saini………………………..…………………………..………
Wadhifa: ……………………………………………………………
Tarehe…………………………………………………………

Lakiri ya Halmashauri ya Moshi imegongwa kwenye sheria Ndogo hii kufutia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Moshi uliofanyika Tarehe 09 Mwezi Februari Mwaka 2021 na Kushudiwa na Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya :-

SHADRACK M. MGAHAGAMA
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Moshi*

MORRIS J. MAKOI
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Moshi*

NAKUBALI,

Dodoma,
5 Decemba, 2023

MOHAMED OMARI MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais,*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*